Policy brief TZ.08/2010K

# Ruzuku ya wanafunzi kwa ajili ya Elimu:

## Ni lini italeta mabadiliko?





## 1. Utangulizi

Serikali lipoanzisha tena elimu ya msingi bila malipo kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) mwaka 2002, ilikuja na ubunifu mmoja muhimu sana: ruzuku kwa kila mwanafunzi. Lengo la msingi la ruzuku hii maalumu kwa kila mwanafunzi ilikuwa ni kuziba pengo la mapato lililotokana na kuondolewa kwa ada. Ruzuku hii pia ililenga kuinua ubora wa elimu kwa kuhakikisha kuwa rasilimali muhimu zinapatikana shuleni. Ililenga hasa kugharami a ununuzi wa vitabu vya kiada na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na kugharamia ukarabati, gharama za utawala na mitihani.

Ruzuku kwa wanafunzi ni kipengele muhimu sana kwenye mpango wa MMEM, na imekuwa ikitengewa rasilimali nyingi: zaidi ya Sh bilioni 80 zilitengwa mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ruzuku hii peke yake. Muhtasari huu unachambua utendaji wa ruzuku hii kwa kina. Imebainika kuwa:

- Sera iliyopitishwa awali ya ugawaji wa ruzuku kwa wanafunzi ya Dola 10 za kimarekani kwa kila mwanafunzi haikuwahi kufuatwa
- Hata kama ingefuatwa, kiwango cha ruzuku kilichowekwa kwa kila mwanafunzi ni kidogo sana kiasi kwamba hakikidhi gharama za vifaa vya kujifunzia.
- Kiwango halisi cha ruzuku hii kinachopelekwa shuleni ni kidogo zaidi ya kile kilichoidhinishwa kwenye bajeti.
- Upelekaji wa fedha za ruzuku shuleni hautabiriki kiasi kwamba haiwezekani kuweka mipango thabiti ya namna ya kuzitumia.

Kutokana na hali hii, tunatoa hoja kwamba ruzuku kwa kila mwanafunzi inahitaji kuangaliwa upya: kwa upande wa sera yake, itengewe fedha zaidi; kuhusu utendaji wake, kiasi cha fedha za ruzuku kinachoidhinishwa kwenye bajeti kinapaswa kutolewa na kupelekwa kikiwa kamili na kwa wakati; na kuhusiana na suala la uwazi, kila mmoja wakiwemo walimu, wazazi na wanafunzi- wanapaswa kufahamu ni kiasi gani cha fedha kitatumwa, lini kinatumwa na kwa madhumuni gani.

Uwazi
pata picha kamili


Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi iliyopo Twaweza/ Hivos Tanzania

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org
Kimetolewa Septemba 2010

## 2. Kuanzishwa kwa ruzuku kwa kila mwanafunzi

Kwa kuziba pengo la mapato ya shule lililotokana na kufutwa kwa ada za shule na michango mbalimbali, kuanzishwa kwa ruzuku hii kumewawezesha watoto wengi toka familia zenye uwezo unaotofautiana kiuchumi kwenda shule. Hii imepunguza tofauti kijamii ya upatikanaji wa elimu kwa wasio na uwezo maana watoto kutoka familia masikini wameweza sasa kwenda shule. Uandikishaji halisi ulipanda kwa kiwango kikubwa, kutoka chini ya asilimia 60 ya wanafunzi wenye umri wa kwenda shule mwaka 2000 hadi kufikia zaidi ya asilimia 95 mwaka 2006 (mchoro 1).

**Mchoro 1: Uwiano wa uandikishaji Halisi, 1995-2009**




| | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 | 1999 | 2000 | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uandikishaji % | 55.4 | 56.3 | 56.7 | 56.7 | 57.1 | 58.8 | 65.5 | 80.7 | 88.5 | 90.5 | 94.8 | 96.1 | 97.3 | 97.2 | 95.9 |


**Chanzo cha data:** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Takwimu za Elimu ya Msingi *Tanzania 2009*.

MMEM imeleta mafanikio mengine pia: madarasa 36,641 yalijengwa kati ya mwaka 2002 na 2006; na kati ya mwaka 2001 na 2009, walimu waliongezeka kwa idadi ya walimu 45,555. Japo idadi ya wanafunzi iliongezeka maradufu, upatikanaji wa vitabu vya kiada pia uliongezeka. Mwaka 2007, uwiano wa kitabu kwa wanafunzi uliripotiwa kuwa 1:3 kulinganisha na ule wa 1:20 mwaka 2000 (Sitta, 2007). Hata hivyo, kigezo cha madai ya mafanikio haya hakiko wazi kwa vile hakuna utafiti wa kina uliofanyika na unaotolewa kama ushahidi kuhusu hali halisi ya upatikanaji wa vitabu.

Awamu ya kwanza ya MMEM (2002-2006) iliyoleta mengi kati ya mafanikio haya ilieleza kwamba ruzuku kwa mwanafunzi kwa kila shule inapaswa kuwa, kwa thamani ya shillingi ya Kitanzania, sawa na dola 10 za kimarekani kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa. Kipindi cha MMEM awamu II (2007-2011), kilipoanza serikali ilipitia upya kiwango cha awali cha Dola ya Kimarekani[1] na ruzuku ikapunguzwa hadi kuwa Sh 10,000, ambayo thamani yake ni chini ya Dola 7 za Kimarekani katikati ya 2010. Mchoro 2 unaonesha mchanganuo wa matumizi ya ruzuku, ukifafanua kiasi gani cha kila shilingi inayopelekwa shuleni inapaswa kutumika kwa ajili ya ukarabati, kununua nyenzo za kujifunzia, vifaa vya ofisini, na pia kusaidia gharama za utawala(kama vile mitihani).

[1] Ingawa MMEM II imedhamiria kuendelea na kiwango cha Dola 10 za kimarekani kwa kila mwanafunzi kama ilivyoahidiwa kwenye MMEM I, kiuhalisia kiasi kinachotegemewa kutolewa kiko kwenye kiambatanisho No. 5 cha MMEM II ambacho kinatoa mgawanyo wa matumizi ya ruzuku kwa mwanafunzi katika Shilingi ya Tanzania kwa jumla ya Sh 10,000.


**Mchoro 2: Mchanganuo wa matumizi ya ruzuku kwa wanafunzi**




**Chanzo cha data:** Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi awamu ya *II 2007-2011.*

Licha ya mafanikio haya, ni vigumu kusema ni kwa kiwango gani ruzuku kwa mwanafunzi imechangia kuboresha elimu. Jambo moja la kukatisha tamaa ni kwamba idadi kubwa ya wanafunzi bado hawana uwezo wa kufaulu Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi. Mwaka 2009, ni asilimia 50 tu ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ndio walifaulu na kupata sifa ya kuendelea na masomo ya sekondari. Vile vile , takwimu za kimkoa zinaonesha tofauti kubwa ya viwango vya ufaulu. Baadhi ya mikoa wanafaulu vizuri mno (kwa kulinganisha na mikoa mingine) wakiwa na kiwango cha ufaulu cha zaidi ya asilimia 70 ya wahitimu. Wakati huo huo mikoa mingine kama vile Shinyanga ina matokeo ya kufadhaisha: ni asilimia 30 tu ya wanafunzi wanaoihitimu ndio wanafaulu (mchoro 3).

**Mchoro 3: Ufaulu wa Mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ki-mkoa mwaka 2008**




**Chanzo cha data:** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Takwimu za Elimu ya Msingi *Tanzania 2009*.

Idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi bila kuwa na sifa za kutosha kuendelea na ngazi za elimu zinazofuata inaibua maswali iwapo MMEM haijengi mfumo wa namna nyingine unaokuza matabaka kulingana na haki za msingi za kijamii wanazostahili na kupata wanafunzi. Inaibua pia swali kuhusu mchango wa ruzuku kwa wanafuzi katika kuongeza ubora wa elimu.

Hata hivyo, kwa kuwa sera ya ruzuku kwa kila mwanafunzi haikutekelezwa kwa namna ilivyotarajiwa, kushindwa kwa mfumo uliopo kuboresha elimu hakupaswi kuchukuliwa kama kiashiria cha kushindwa kwa ruzuku kwa wanafunzi. Bila kutekelezwa vizuri, ruzuku inayotolewa haiwezi kutarajiwa kuzaa matunda na kuleta tija.

## 3. Mambo nane kuhusu ruzuku kwa wanafunzi

Data kuhusu utoaji ruzuku katika Halmashauri za Wilaya na kwenye ngazi ya shule hazipatikani kiurahisi, na hili ni jambo la kushangaza. Kwa vile ruzuku ya wanafunzi ni fedha za wananchi zenye lengo la kuboresha mafunzo wanayopata shuleni, ni haki ya wananchi kwamba taarifa kama hizo zipatikane kiurahisi kwa umma. Serikali pia itafaidika wananchi wanapopata taarifa hizo, maana ufuatiliaji ni muhimu katika kusaidia uandaaji wa mipango bora. Kwa hiyo, kuna hitaji la haraka la kuwa na mfumo makini wa kufuatilia na kutoa taarifa za kiasi cha ruzuku ya wanafunzi kinachotolewa kutoka serikali kuu kwenda Halmashauri na kutoka Halmashauri kwenda shuleni.


Wakati taarifa hizi bado hazipatikani, muhtasari huu unachambua taarifa zilizotokana na ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za umma *(Public Expenditure Tracking Survey)* wa sekta ya elimu, vitabu vya bajeti, na mahojiano yaliyofanywa na baadhi ya walimu. Mambo yafuatayo yaligundulika na yanahitaji kuangaliwa kwa makini.

### 3.1 Tangu mwaka 2002 thamani ya ruzuku kwa mwanafunzi ilishuka kwa zaidi ya 35%

Wakati wa awamu ya kwanza ya elimu bila malipo, chini ya MMEM I (2002-2006), Sera ya ruzuku kwa wanafunzi ilisema kiwango cha ruzuku kitakuwa ni Dola 10 za Kimarekani kwa kila mwanafunzi kwa mwaka. Sera hii ilibadilishwa kuwa Sh 10,000 katika MMEM II (2007-2011).

Kati ya mwaka 2001 na 2009 gharama za maisha nchini Tanzania ziliongezeka kwa kiwango kikubwa. Mwaka 2002 Sh 593 iliweza kununua bidhaa zilizonunuliwa kwa Sh 1,000 mwaka 2009 (NBS, 2009). Wakati wa awamu ya kwanza ya MMEM (kati ya mwaka 2002 na 2006), ruzuku ya wanafunzi ililindwa dhidi ya kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania maana ilikuwa inakokotolewa kwa Dola ya Kimarekani. Lakini sera ilipopitiwa upya chini ya MMEM II, thamani halisi ya ruzuku ya wanafunzi ilishuka haraka. Mwaka 2002, Ruzuku ya Dola 10 ilikuwa na thamani sawa na Sh 9,666 za kitanzania. Mwaka 2009, ruzuku ya Sh 10,000 iliyopangwa ilikuwa na thamani halisi ya Sh 6,078 tu (ikiangaliwa kwa thamani ya Sh mwaka 2002 ), huku ni kushuka kwa thamani kwa asilimia 37 (mchoro 4).

**Mchoro 4: Sera ya ruzuku kwa wanafunzi kwa thamani halisi ya shilingi , 2002-2009**[2]




**Chanzo cha data:**Ukokotozi wa mwandishi kwa kuzingatia kiasi cha ruzuku kwa wanafunzi kilichotajwa na MMEM

Kwa kuweka sera ya ruzuku kwa wanafunzi isiyobadilika kulingana na mabadiliko ya thamani ya fedha, serikali imeruhusu thamani ya ruzuku kwa wanafunzi kufifia kwa namna ambayo inaibua maswali kuhusu dhamira ya serikali kufikisha rasilimali karibu zaidi na jamii . Mwenendo huu unakatisha tamaa ukizingatia kuwa bajeti ya sekta ya elimu imeongezeka kwa kiwango kikubwa tu miaka ya hivi karibuni.

Lakini, hata bila kuangalia kushuka kwa thamani ya fedha kulikotokana na mfumuko wa bei, kiasi halisi cha fedha kinachozifikia shule kwa ajili ya ruzuku kwa wanafunzi ni wazi kiko chini zaidi leo, ukilinganisha na kiasi kilichokuwa kikifika kati ya mwaka 2002 na 2003. Kwa mujibu wa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika sekta ya elimu wa mwaka 2004, katika kipindi cha mwaka 2002-2003 shule zilipokea wastani wa Sh 5,400 kwa kila mwanafunzi. Hata hivyo, mwaka 2007/08, fedha halisi iliyofika shuleni ilipungua na kuwa Sh 4,189 kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa (URT, 2010). Hili linaweza kuwavutia wengi kulifahamu hasa walimu na wananchi, ambao wana nia ya kuhakikisha kwamba rasilimali za kutosha zinapatikana kwa ajili ya kufanikisha ubora mashuleni.

## 3.2. Ruzuku kwa wanafunzi haitoshi kununulia idadi inayokidhi ya vitabu vya kiada

Kiasi cha ruzuku kinachotolewa kwa ujumla kimeshuka, lakini kina thamani gani kwa sasa? Je, kinatosha kugharimia mahitaji muhimu? Pata picha ya nini kinaweza kununuliwa na kiasi hicho cha fedha. Kama inavyooneshwa kwenye mchoro 2, asilimia 40 au Sh 4,000 ya ruzuku iliyopangwa kwa mwanafunzi ni ya kununulia vitabu vya kiada na viongozi vya walimu kwa masomo yote, yakiwemo masomo ya Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Uraia, stadi za kazi, n.k. Ukitizama orodha ya bei ya vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa kufundishia, kwa kuchukua mfano wa orodha ya bei za vitabu za kampuni moja (Ben and Company Limited mwaka 2008-2009), pesa hii inairuhusu shule kununua, si zaidi ya kitabu kimoja tu kwa kila mwanafunzi. Hii ni kwa kuwa bei za vitabu ziko kati ya Sh 3,500 na 5,000. Kuna vitabu pia ambavyo bei yake ni ghali zaidi.

Kama mtoto anasoma masomo 6, vinahitajika si chini ya vitabu sita, ambavyo vitapatikana kwa gharama ya Sh 38,900. Chukulia kuwa vitabu vinadumu kwa miaka mitatu (makadirio haya ni ya juu kwa vitabu vinavyotumika sana), mgawo wa Sh 13,000 kwa mwaka ungehitajika kwa ajili ya vitabu tu. Hivyo, hata kama kiasi cha ruzuku kwa wanafunzi cha Sh 10,000 kwa kila mwanafunzi

[2] Dola ya Kimarekani inabadilishwa kwenda Shilingi kwa kuzingatia wastani wa viwango vya kubadilisha fedha vya mwaka.

kingekuwa kinapelekwa na kufika chote shuleni, (kitu ambacho hakifanyiki) kiasi cha Sh 4,000 kingekuwa pia hakitoshi kabisa kununulia idadi inayohitajika ya vitabu vya kiada.

**Jedwali 1: Fungu la ruzuku kwa wanafunzi kulinganisha na gharama halisi za vitabu vya darasa la 5**


| Vitabu vinavyohitajika (darasa la 5) | Bei ya kitabukwa Shs |
|---|---|
| Kitabu cha Historia darasa la 5 | 4,900 |
| Kitabu cha jiografia darasa la 5 | 4,800 |
| Kitabu cha Uraia darasa la 5 | 4,800 |
| Kitabu cha Hisabati darasa la 5 | 4,900 |
| Kitabu cha Kiswahili darasa la 5 | 5,200 |
| Kitabu cha kiingereza darasa la 5 | 4,900 |
| Kitabu cha Sayansi darasa la 5 | 4,500 |
| Kitabu cha Stadi za kazi darasa la 5 | 4,900 |
| **Gharama halisi kwa jozi ya vitabu vya darasa la 5** | **38,900** |
| **Fungu la vitabu (40%) ruzuku kwa kila mwanafunzi** | **4,000** |
| **Fungu la vitabu kama % ya mahitaji halisi** | **10.2%** |

**Chanzo cha data:** Ruzuku kwa wanafunzi: Bajeti ya 2009/10; Orodha ya bei za vitabu: Ben and Company Limited, *Katalogi ya Shule za Msingi Tanzania Jan 2008-Des 2009.*

## 3.3 Kiasi kilichotengwa katika bajeti ni kidogo kuliko kilichotajwa na sera ya MMEM

Kiasi kilichotengwa katika bajeti kwa ajili ya ruzuku ya kila mwanafunzi kimekuwa chini kwa mfululizo kuliko kiasi kilichosemwa kwenye sera ya MMEM kilichokubaliwa na Baraza la Mawaziri. Mwaka 2007/08, kwa mfano, mapungufu katika ruzuku kwa kila mwanafunzi yalikuwa ni Sh 4,481 maana serikali ilitenga Sh 5,519 kwa kila mwanafunzi ukilinganisha na kiasi cha Sh 10,000 kwa kila mwanafunzi kilichosemwa kwenye sera. Mchoro 5 hapo chini unaonesha mapungufu ya fedha inayotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya ruzuku kwa kila mwanafunzi kwa kipindi cha miaka minne iliyopita.[3]

**Mchoro 5: Upungufu wa ruzuku kwa kila mwanafunzi katika bajeti ya mwaka 2006/07-2009/10**




**Chanzo cha data:** ukokotozi wa mwandishi kwa kuzingatia data za bajeti.


[3] Ukokotozi wote wa ruzuku kwa wanafunzi kwa mwaka wa fedha unazingatia kuwa ruzuku kwa wanafunzi inapangwa kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi walioandikishwa kwa mwaka huo wa kalenda. k.v, mgawo katika mwaka 2007/08 ulizingatia idadi ya wanafunzi walioandikishwa mwaka 2007.

## 3.4. Kuna maboresho yanayofanyika

Kama ilivyooneshwa kwenye mchoro 5, kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya ruzuku kwa kila mwanafunzi (katika bajeti, sio kile kiasi kilichopokelewa shuleni, angalia 3.6 hapo chini) kiliongezeka kwa mwaka 2009/10. Mwaka 2008/09 iliidhinishwa kama Sh 6,851 kwa kila mwanafunzi, au pungufu ya Sh 3,149 kwa kiwango cha sera. Katika mwaka 2009/10 kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti kilikuwa ni Sh 9,627, ikiwa ni pungufu kwa sh 373 tu kufikia kiwango cha sera.

Wakati tarakimu hizi za jumla zinaonesha maboresho muhimu, kwenye ngazi ya Wilaya bado hali ni ileile zikiwepo Wilaya zilizoidhinishiwa viwango vilivyo tofauti sana na wastani. Mchoro 6 unaonesha ruzuku kwa wanafunzi iliyoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2009/10 kwa Halmashauri zote za Wilaya. Unaonesha namna ambavyo wastani wa kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ulivyo karibu Sh 10,000 kwa kila mwanfunzi. Hata hivyo, kuna Halmashauri ambazo ziliidhinishiwa kiasi ambacho ama ni kikubwa zaidi, au kidogo zaidi ya wastani wa kwenye bajeti. Halmshauri za mkoa wa Iringa zipo kwenye kundi la chini zaidi: ni miongoni mwa Halmashauri 10 zilizoidhinishiwa kiwango kidogo zaidi cha ruzuku, wakati Mafia (mkoani Pwani) na Sikonge (Tabora) ziko juu zaidi.

**Mchoro 6: Ruzuku kwa wanafunzi kwa mujibu wa maidhinisho ya bajeti kwa mwaka 2009/10**




**Chanzo cha data:** ukokotozi wa mwandishi kwa kuzingatia data za bajeti ya 2009/10.


## 3.5. Tofauti kwenye maidhinisho ya bajeti haziashirii upendeleo kimkoa

Kuhusu maidhinisho ya ruzuku ya wanafunzi , tulichunguza data ili kuona kama Mikoa iliyo na hali nzuri kiuchumi siku zote inapata kiasi kikubwa cha ruzuku kuliko mikoa masikini. Hali ya kiuchumi kimkoa inatofautiana kwa kiwango kikubwa hapa nchini. Taarifa za Idara ya Takwimu (NBS) ya Taifa zinaiweka Dar es Salaam kwenye nafasi ya juu kiuchumi na Singida nafasi ya chini kabisa kwa kuzingatia wastani wa kipato cha mtu mmoja mmoja kwa mikoa katika mwaka 2008.

Kwa kuangalia taarifa juu ya maidhinisho ya ruzuku ki-mkoa kwa mwaka 2008/09 na 2009/10 (mchoro 7), tunaweza kuona kuwa ruzuku haitolewi kwa mfumo unaoelezeka. Wakati fulani mikoa ambayo ina hali ngumu kiuchumi inawekewa kiasi kidogo cha ruzuku kwa kila mwanafunzi kuliko mikoa yenye hali nzuri zaidi kiuchumi. Lakini, pia kuna nyakati ambapo mikoa yenye vipato vidogo inatengewa rasilimali nyingi zaidi ya mikoa iliyo na hali nzuri kiuchumi. Kwa mujibu wa

takwimu za NBS kuhusu pato la mwananchi mwaka 2008, Singida na Dodoma zina kipato kidogo zaidi. Mwaka 2008/09, mikoa hiyo miwili ilikuwa pia ni miongoni mwa mikoa 5 iliyopangiwa kiasi kidogo sana cha ruzuku kwa kila mwanfunzi, ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam na Kilimanjaro (mikoa ambayo ina kipato kikubwa kabisa) na Morogoro (mkoa wenye kipato cha kati). Kwa hali hii, mtu hawezi kwa ujasiri kusema kwamba mikoa iliyo imara kiuchumi inapendelewa kwenye maidhinisho ya bajeti ya ruzuku kwa wanafunzi.

**Mchoro 7: Maidhinisho ya ruzuku kwa wanafunzi kimkoa mwaka 2008/09 na 2009/10**




**Chanzo cha data:** ukokotozi wa mwandishi kwa kuzingatia data za bajeti kwa mwaka wa fedha 2008/09 na 2009/10.


## 3.6. Sio fedha zote zinazoidhinishwa kwenye bajeti zinapokelewa shuleni

Ili ruzuku kwa wanafunzi ilete matokeo, fedha zinapaswa kufika shuleni. Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma ni zana nzuri ya kutathmini iwapo fedha zinazotengwa kwa ajili ya ruzuku kwa wanafunzi kweli zinafika shuleni.

Hivi karibuni, kwa kushirikiana na Wahisani wake, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliidhinisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma ufanyike kwa mwaka wa fedha wa 2007/08. Uchunguzi huu unafichua kuwa, mgawo wa fedha za ruzuku uko chini ya kiwango kilichotajwa na sera, pia sio fedha zote zilizotengwa zinafika shuleni. Mkoa, Halmshauri ya Wilaya, au shule inaweza kupokea zaidi au pungufu ya kiwango ilichoidhinishwa; lakini mara nyingi wanapokea pungufu.

Kwa mfano, mwaka 2007/8 kiasi cha ruzuku kwa wanafunzi kilichofika shuleni kilikuwa kwa wastani Sh 4,189 kwa mtoto, wakati Halmshauri za Wilaya ziliripoti kutoa ruzuku ya wastani wa Sh 4,570 kwa kila mwanafunzi (MoEVT, 2010). Bado, kiwango hiki kikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa mwaka huu unakuta kwamba zilitengwa Sh 5,519 kwa kila mwanafunzi (mchoro 8). Uchunguzi wa *PETS* ulibaini tofauti zaidi kwenye ngazi ya Halmashauri na shule, kwa kuonesha kwamba kiasi halisi kilichotolewa kilikuwa kati ya Sh 1,260 (kiasi cha chini kabisa) na Sh 19,236 kwa kila mwanafunzi.

**Mchoro 8: Ruzuku kwa wanafunzi mgawo halisi na upelekaji ikilinganishwa na Sera ya MMEM mwaka 2007/08**




**Chanzo cha data:** Mgawo wa bajeti (Data za bajeti); Utoaji fedha (Halmshauri) & mpokeaji (Shule): URT (2010) Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwa elimu ya msingi na Sekondari Tanzania Bara, Ripoti ya mwisho Februari 2010.

***Kisanduku 1: Uzoefu wa Mwalimu kuhusu ruzuku kwa mwanafunzi***

*"Tunapokea ruzuku kwa kila mwanafunzi, lakini ni kiasi kidogo sana kulinganisha na gharama halisi, pia ni kiasi kidogo katika MMEM awamu hii kuliko kipindi cha MMEM I. Mwaka jana, kwa mfano, shule yangu ilipokea kama Sh 4,500 kwa kila mwanafunzi. Na licha ya hilo, kiasi hicho kinakuja katika mafungu madogomadogo kiasi ambacho inatuwia vigumu kupanga manunuzi. Mwezi Desemba mwaka jana kwa mfano, tulipokea Sh 187,000. Je, fedha hizi zingenunua nini kwa ajili ya wanafunzi wangu 427?*

*Kwa sasa uwiano wa vitabu kwa wanafunzi shuleni kwangu ni 1:7. Wazazi hawashiriki kununua vitabu vya ziada kwa ajili ya watoto wao. Ukweli ni kwamba hali hii ni ngumu kushughulika nayo. Huwezi kuwaagiza wanunue vitabu, hawataelewa,na hata ungewaagiza kununua hawawezi kufanya hivyo kwa sababu wameaminishwa kuwa serikali inalipia gharama hizo. Hivyo, tunafanyia kazi kile tunachopata. Zaidi ya hayo, upatikanaji wa walimu nao ni tatizo.*

*Likija suala la mitihani, kwa kweli wanafunzi wanapaswa kufaulu, na wanafanya vizuri tu. Lakini ngoja nikuambie—naweza kukuhakikishia kwamba ufaulu mzuri katika hali kama hii unawezekana tu kwa sababu kuna udanganyifu mwingi unaoendelea.*

*Ninachoweza kupendekeza ni kwamba ofisi za Maafisa elimu Wilaya zirudishiwe jukumu la kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Uzoefu unaonesha kwamba kuna wakati fulani fedha zinatumiwa vibaya au vitabu vinavyonunuliwa vinakuwa vya ubora duni."*

*Mwalimu Mkuu Shule mojawapo ya Msingi, Wilayani Rorya*

## 3.7. Muda wa utoaji ruzuku kwa wanafunzi haueleweki

Kwa madhumuni ya kufanikisha mipango, muda wa kutolewa kwa ruzuku ya wanafunzi unapaswa kujulikana; kiasi kinachotolewa kinapaswa kuwa cha uhakika na fedha zifike kwa wakati.
Fedha inayofika shuleni mwishoni mwa mwaka wa shule haiwezi tena kutumika kuwanufaisha wanafunzi. Kwa bahati mbaya, ucheleweshwaji wa ruzuku ya wanafunzi, na ruzuku kufika kwa mafungu madogomadogo badala ya kwa kiwango kamili, inaonekana kuwa kama ni kanuni.

***Kisanduku 2: Uzoefu wa Mwalimu kuhusu ruzuku kwa wanafunzi***

*"Tuna wanafunzi zaidi ya 1,000 hapa shuleni. Na kwa sasa tuna jumla ya walimu 16. Tunapata ruzuku ya mwanafunzi, lakini inaletwa kwa mafungu na wakati fulani inacheleweshwa sana. Mbali na hilo, haitoshi. Tunachofanya ni kwamba tunawaomba wauzaji wa vitabu kutuuzia vitabu kwa mkopo na tunawalipa fedha zikija. Tunashukuru wanatuelewa na kutuamini kwamba tutawalipa.*

*Bei za vitabu zinatofautiana. Kwa mwaka jana, kwa mfano, kitabu cha bei ndogo zaidi kiliuzwa sh 3000; kwa wastani bei ya kitabu ni sh 5,800. Kwa sababu hatuwezi kununua vitabu vya kutosha wanafunzi wanalazimika kuchangia vichache tulivyonavyo. Kwa sasa uwiano wa kitabu kwa wanafunzi kwa baadhi ya madarasa ni 1:5, na madarasa mengine ni 1:6. Wanalazimika kutumia vitabu wakati wa vipindi tu, vipindi vikiisha tunavikusanya ili wengine nao waweze kuvitumia. Hawawezi kwenda na vitabu nyumbani. Baadhi ya wazazi wanaoweza kumudu gharama za vitabu wanawanulilia vitabu watoto wao. Lakini wengi hawanunui.*

*Mwaka unapoanza, nakuwa sijui nitapokea shilingi ngapi. Ninasubiri kile watakachotutumia. Na kwa sababu sijui tutakachotumiwa, siwezi pia kukidai."*

*—Mwalimu Mkuu wa shule mojawapo ya msingi, Dar es Salaam*

Walimu WAkuu waliohojiwa hawakuwa wanajua ni lini na ni kiasi gani shule itapokea kama ruzuku kwa wanafunzi. Hali hii ina maana kuwa hata kama wakipokea kiasi kidogo kuliko kile wanachostahili kupata, hawatajua. Kwa hali hiyo, hawako kwenye nafasi ya kufuatilia sera inasema nini kuhusu kile wanachostahili.

## 3.8. Usimamizi ni dhaifu—fedha pekee hazitatatua matatizo

Bila kuwa na usimamizi wa kutosha uhakika ni mdogo kuwa rasilimali zitatumika kama zilivyokusudiwa. Pengo kati ya sera na maidhinisho ya bajeti, kati ya bajeti inayoidhinishwa na fedha inayotolewa, na hadithi kama ilivyo kwenye kisaduku 1 vinaonesha kuwa fedha zinaweza kuishia kutumika vibaya kiurahisi tu. Suala hili linathibitishwa na kile kinachoelezwa katika *Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya watu (Poverty and Human Development Report)* (2009) kuhusu mfumo dhaifu wa manunuzi ya vitabu vya kiada. Ripoti iliongelea suala muhimu lililoibuliwa na *Mapitio ya Sekta ya Elimu 2008* kuhusu idadi kubwa ya vitabu ambavyo havinunuliwi licha ya fedha kupelekwa shuleni au vinanunuliwa lakini vinawekwa kwenye makabati wakati wanafunzi wanahitaji kuvisoma. Pia iligundua matatizo ya wizi kwa njia ya unakili usio halali (*pirating*) na ubora duni wa nakala za vitabu vilivyoidhinishwa na vinavyotumiwa mashuleni.

Usimamizi makini unahitajika katika nyanja zote nne ambazo ni muhimu kwenye mafanikio ya ruzuku kwa wanafunzi:

- Maidhinisho ya bajeti,
- Mgawo wa fedha ,
- Muda wa mgawo/kutumwa fedha, na
- Utumiaji fedha.

Suala hili la mwisho halijajadiliwa hapa, lakini ni wazi kwamba kama fedha zinafika shuleni, wazazi kupitia kamati za shule wanaweza kuchukua jukumu la kusimamia matumizi.

## 4. Hitimisho

Ruzuku kwa wanafunzi imechangia ongezeko kubwa la uandikishaji shule wa wanafunzi na imesaidia kupunguza upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Wakati huohuo, bado inakatisha tamaa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza shule za msingi wasioweza kufaulu mtihani wa mwisho wa elimu ya msingi . Na wakati tofauti za upatikanaji wa elimu kwa makundi mbali mbali ya jamii zimetatuliwa kwa kiasi kikubwa tofauti mpya kwenye ujenzi wa uwezo na ujuzi zinaonekana kuibuka.

Muhtasari huu umegundua kuwa sera ya ruzuku kwa wanafunzi haiendani na/ haijazingantia hali halisi ya uhitaji. Mathalani, kiwango cha ruzuku kilichosemwa na sera kiko chini mno kikilinganishwa na kiasi kinachohitajika kununulia walau vifaa vichache vya msingi vya kujifunzia vinavyohitajika. Pia, imeonekana kuwa namna ambavyo mfumo wa ruzuku unatekelezwa unaacha mapungufu mengi yanayohitaji kutatuliwa: kiasi kinachoidhinishwa kwenye bajeti ni kidogo kuliko kiwango kilichoelezwa na sera, kiasi kinachotengwa kwa ajili ya Wilaya hakifuati vigezo rasmi, kiasi kamili kilichoidhinishwa kwenye bajeti hakitolewi, na si chote kinachotolewa kinafika shuleni. Fedha zinatumwa shuleni kwa mafungu madogo madogo na usimamizi ni dhaifu kwenye mfumo mzima.

Elimu ya watoto wa Kitanzania ni muhimu sana na kuruhusu haya yaendelee kutokea kunadhoofisha utoaji elimu bure ya msingi kwa watoto wote. Wito wa kufanya mabadilika katika mfumo wa sasa wa ruzuku kwa wanafunzi unatolewa. Mabadiliko yanaweza kuanziaa kwenye maeneo kadhaa.

- Kwanza, ili sera izae matunda, inahitaji kuzingatia hali halisi ya uhitaji uliopo. Kiasi cha ruzuku kwa wanafunzi cha Sh 10,000 kama kilivyosemwa na MMEM II ni kidogo sana hata kutegemewa kuleta mabadiliko ya maana katika kuboresha elimu. Kinahitaji kupitiwa upya na kuongezwa.
- Pili, sera inapoundwa inapaswa kutekelezwa kwa vitendo. Kiasi kamili cha ruzuku kwa wanafunzi kilichotamkwa kwenye sera kinapaswa kufika shule, kwa viwango vinavyotabirika na kwa wakati.
- Tatu, usimamizi na uwazi kuhusu maidhinisho na mgawo wa ruzuku kwa wanafunzi, utumaji wa fedha, na utumiaji fedha vinahitaji kuboreshwa zaidi. Serikali (kuu na za mitaa) zinapaswa kutangaza ruzuku ya wanafunzi inayotolewa kwa ujumla wake na kwa kila mwanafunzi mwaka unapoanza. Shule zinapaswa kuripoti kwa uwazi ruzuku waliyopokea, na jinsi fedha zilivyotumika, kwa namna ambayo iko wazi na inaeleweka kwa kila mzazi, mwalimu na mwanafunzi.

## Rejea


Ben & Company Limited (2008). *Katalogi ya Shule za Msingi Tanzania, Jan 2008-Des 2009.* Dar es Salaam: Ben & Company LTD.

National Bureau of Statistics (NBS) (2009). *Consumer Price Index for November 2009*. Retrieved February 20, 2010, from Government of Tanzania: http://www.nbs.go.tz/index.php?option =com_phocadownload&view=category&id=67:inflation&Itemid=106.

Osei, Robert D, Getrude A. Owusu, Freda E. Asem, and Robert L. Afutu-Kotey (2009). *Effects of Capitation Grant on Education Outcomes in Ghana.* Retrieved February 15, 2010, from Institute of Statistical and Economic Research (ISSER): www.gdnet.org/CMS/getFile.php?id=undp_**isser**1.

Sitta, Margaret S. (2007) "Towards universal primary education: the experience of Tanzania". UN Chronicle. Retrieved February 15, 2010, from FindArticles.com: http://findarticles.com/p/articles/mi_m1309/is_4_44/ai_n25356881/.

URT (2005, 2007, 2009). *Basic Education Statistics in Tanzania.* Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training (MoEVT).

URT (2002, 2007) *Primary Education Development Programme Document*. Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training.

URT (2006, 2007 2009). Budget Speech. Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training.

URT (2004). Public Expenditure Tracking Survey of Primary Education 2002-2003 (unpublished).

URT (2010). *Public Expenditure Tracking Survey of primary and secondary Education in Mainland Tanzania, Final report, February 2010*. Dar es Salaam, Ministry of Education and Vocational Training